

Mdau wa maendeleo,

Clion Odhiambo Dismas,

Mawasiliano: simu +255684693094

: barua pepe odhiamboclion@gmail.com/ clionodhiambo@yahoo.com

21/09/2017.

Kwa,

Mkuu wa mkoa Mara,

S.l.p 299,

Musoma-Mara.

Barua pepe: ras@mara.go.tz

Ndugu,

YAH: OMBI LA UKUBALI WA UJENZI CHUO KIKUU MKOANI KWAKO MARA.

Husika na kichwa tajwa hapo juu, mimi ni mdau wa elimu, mwenyeji wa mkoa wa MARA, kwa taaluma ni mhandisi wa umeme, kwa majina CLION ODHIAMBO DISMAS, kijana wa miaka 25. Ninawiwa na kunuia kuanzisha kampeni ya ujenzi wa chuo kikuu hapo katika mkoa wako ambako ndiko nyumbani kwangu.

Aidha , ninaelewa fika yumkini serikali uwenda ina mpango huu tangu zamani lakini kulingana na kipaumbele na malengo yake, labda kwa baadae watafanya ivyo. Lengo langu kubwa ni kuhamasisha ujenzi wa chuo kikuu mkoa mzima, nyumba kwa nyumba, mtaa kwa mtaa, kata kwa kata, tarafani, wilayani, ngazi ya mkoa, kitaifa na kimataifa. Watu wana pesa na watu wako tayari kuona maendeleo ya kitaaluma ambayo katika serikali ya viwanda, itachochea kupata wataalamu wazalendo wengi watakao kuja kujenga uchumi wa taifa letu hili.

Baada ya kupitia data zilizotumika katika ujenzi wa vyuo vikuu kama DODOMA na MLOGANZILA, tawi la Muhimbili, nimekuja na tathmini ya fedha za kitanzania shilingi bilioni 224, ambazo ni sawa na dola milioni 100 za kimarekani. Uwezo wake utaweza kudahili wanafunzi takribani elfu kumi na Zaidi kwa mkupuo. Amabapo mara ni karibia eneo la mraba elfu thelatini na wakaazi Zaidi ya milioni moja na laki saba kwa sense ya watu na makazi yam waka 2012.

Ninaomba kibali cha kufanya jambo hili, takribani hekari elfu kumi(10000) kwa maana, bila ya ardhi au sehemu ya kujengea, nitakapo zunguka kwa watu na taasisi nyingi katika ngazi ya kitaifa hata kimataifa, sitaweza kufanikiwa katika jambo hili. Ninaamini serikali yangu ni sikivu na inayopenda maendeleo katika taifa lake ila ya kujadi dini, itikadi wala rangi za raia wake. Ninatanguliza shukrani na kazi njema.

Aidha, kuhusu ufafanuzi wa jambo hili utafanyikaje, niko tayari kuelezea endapo nikihitajika kufanya hivyo.

Clion O dismas

A handwritten signature in black ink, appearing to be 'Clion O dismas', written over a horizontal dotted line.

NAKALA

ofidi ya rais- ikulu,

S.l.p 11400,

Dar es salaam.

Barua pepe ikulu@ikulu.go.tz

Ofisi ya waziri mkuu(UDOM),

S.l.p 980,

Dodoma.

Barua pepe ps@pmo.go.tz

Ofisi ya waziri wa elimu, sayansi na teknolojia(UDOM),

S.l.p 10,

Dodoma.

Barua pepe info@moe.go.tz